JULACE: Journal of University of Namibia Language Centre
Volume 5, No. 1, 2020 (ISSN 2026-8297)

# Ufasiri wa Mahusiano ya Uwakati Baina ya Vishazi Ambatani katika Lugha ya Kiswahili

Luinasia E. Kombe[1]
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam*

**Abstract**
Apart from forms that make the temporal relation explicit in coordinate structure, such as temporal connectives and adverbial of time, language has different ways of signalling that relation without using those forms. This paper intends to analyse how temporal pragmatic relations signalled between clauses which are linked by the coordinator *na* 'and' in Kiswahili. The study relies on Relevance Theory (cf. Sperber & Wilson 1986, Wilson & Sperber 2004) which is human cognition and communication theory. Using data from literature publications, speeches, government reports, and magazines, this paper reveals that coordinator *na* 'and' does not express temporality between coordinated clauses, as opposed to *and* in the English language (cf. Carston 2002). The paper shows that temporality relation in Kiswahili is expressed by *-ka-* tense affix and *ku-* infinitive affix.

**Ikisiri**
Mbali na kuwapo kwa maumbo yanayobainisha mahusiano ya wakati kama vile viunganishi vya wakati na vielezi vya wakati, lugha zina namna nyingine anuwai za kudhihirisha mahusiano hayo bila kutumia maumbo hayo. Makala haya yanalenga kufafanua namna mahusiano ya kipragmatiki ya uwakati yanavyoashiriwa baina ya vishazi ambatani vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi ambatanishi *na* pasipo matumizi ya vielezi vya wakati au viunganishi vya wakati katika lugha ya Kiswahili. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Uhusiano (taz. Sperber & Wilson 1995, Wilson & Sperber 1993, 2004) ambayo ni nadharia ya utambuzi wa binadamu na mawasiliano. Data za utafiti huu zimepatikana katika machapisho ya fasihi, hotuba na ripoti za serikali na magazeti. Matokeo ya makala haya yanaonesha kuwa kiunganishi ambatanishi *na* hakina dhima ya kipragmatiki ya kuashiria mahusiano ya uwakati, baina ya vishazi ambatani kama ilivyo kwa kiunganishi '*and*' katika Kiingereza (taz. Carston 2002). Badala yake mahusiano hayo katika lugha ya Kiswahili huashiriwa kwa kiambishi njeo *-ka-* na kiambishi kisoukomo *ku-*

## Utangulizi

Kiunganishi ambatanishi *na* ni miongoni mwa viunganishi ambatanishi vinavyoambatanisha virai na vishazi katika lugha ya Kiswahili. Katika makala haya vishazi ni tungo zote zenye vitendo yaani sentensi, vishazi vyenyewe na virai vitenzi. Katika makala haya tungo hizo zimeitwa vishazi kwa sababu katika mazingira mengi, ni vigumu kutofautisha virai vitenzi, vishazi na sentensi kwa kuwa huingiliana. Hoja hii inaungwa mkono na Haspelmath (2004:8) kwamba virai vitenzi, vishazi na sentensi huwekwa pamoja kwa sababu haijawa wazi ni kigezo gani kinaweza kutumika kuvitofautisha.

Mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyobebwa na vishazi ambatani huoneshwa kwa kwa uwazi kwa kutumia viunganishi ambatanishi vya uwakati (Mithun, 1988; Haspelmath, 2000, 2004; Kombe, 2019). Mathalani, Kombe (2019) anaeleza kuwa, viunganishi ambatanishi vinavyoonesha mahusiano ya uwakati katika lugha ya Kiswahili ni *kisha* na

---

[1] Luinasia Elikunda Kombe is a lecturer in the Faculty of Humanities and Social Sciences at the Dar Es Salaam University College of Education (DUCE). Luinasia's research areas of interest include Africal Languages, Kiswahili grammar, sociolinguistics, and comparative linguistics. Email: kombeluinasia@gmail.com

*halafu*. Mifano (1-2) inafafanua zaidi namna viunganishi hivyo namna vinavyounganisha matukio kiuwakati.

(1) Aliniamuru [[nimpe leseni], **kisha** [niegeshe gari langu pembeni]]. (Mtanzania 30/4/2017:3)
(2) Hatuwezi kuwa na watu wanajiita wawekezaji [[tunawapa viwanda vyetu] **halafu** [wanaviatamia tu]]. (Magufuli 20/11/2015:10)

Kiunganishi *kisha* katika mfano (1) hapo juu kinatoa fasiri kuwa tendo la kumpa leseni na tendo la kuegesha gari pembeni yanahusiana kiwakati. Tendo la kishazi cha pili linafuata kiwakati baada ya tendo la kishazi cha kwanza. Pia, kiunganishi *halafu* katika mfano wa (2) kinatoa fasiri kuwa kitendo cha kuwapa viwanda vyetu kilianza kikafuatiwa kiwakati na kitendo cha kuvitumia. Hivyo, viunganishi ambatanishi *kisha* na *halafu* ni viunganishi ambatanishi vinavyoonesha mahusiano ya uwakati baina ya matukio ndani ya tungo ambatani.

Aidha, makala haya hayashughulikii mahusiano hayo ya uwakati yanaooneshwa kwa uwazi na viunganishi vya uwakati bali yanachunguza tungo ambatani kuanzia sasa (TUA) ambazo hazina viunganishi hivyo, lakini bado msikilizaji au msomaji anaweza kupata fasiri ya mahusiano ya uwakati yaliyopo baina matukio yaliyobebwa na vishazi ambatani. TUA zinazochunguzwa katika makala haya ni zile zenye kiunganishi ambatanishi ongezi *na*. Makala haya yanalenga kuonesha kuwa mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatanishi vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi ambatanishi ongezi *na* hayaashiriwi na kiunganishi hicho. Hali hii ni kinyume na ilivyobainishwa na baadhi ya wataalamu kama Levinson (2000), Carston (2002), Amfo (2007, 2011) na Nartey (2018) kwamba kiunganishi chenye semantiki sawa na *na* katika lugha walizotafiti huashiria mahusiano ya uwakati.

**Nadharia ya Uhusiano**

Makala haya yanatumia Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Wilson na Sperber (1986); (2004). Nadharia hii inachunguza zaidi madai ya Grice (1967) kuhusu umuhimu wa udedushi katika mchakato wa ufasiri wa maana. Tofauti na Grice, Wilson na Sperber wana mtazamo kwamba mchakato wa kipragmatiki ni wa muhimu katika kumsaidia mshiriki wa mazungumzo kupata maana iliyowasilishwa kwa uwazi na ile isiyowasilishwa kwa uwazi. Nadharia ya Uhusika inadai kwamba msikilizaji au msomaji watafuta maana katika muktadha wowote wa mawasiliano na baada ya kupata maana inayoendana na matarajio yao ya uhusiano wataacha kuchakata. Nadharia hii inalenga kueleza mbinu inayotumiwa kung'amua maana isiyodhahiri kutokana na vidokezo vya kimuktadha vilivyoko kwenye matini au usemi. Forceville (2005;2014) anaeleza kuwa, mwanzoni Nadharia hii ya Uhusiano kwa kiasi kikubwa ilitumika katika ufafanuzi wa mawasiliano ya mdomo lakini kwa sasa hutumika pia katika njia nyingine za mawasiliano.

Kwa mujibu wa nadharia hii, usemi unahusika kwako, kama unaendana kwa namna fulani na dhana au nadharia zilizopo kuhusu ulimwengu. Uhusiano unafasiliwa kwa kuhusisha jitihada za kuchakata maana na athari za kimuktadha. Hivyo, usemi unahusika unapoungana na mabunio ya kimuktadha kuleta athari za kimuktadha. Athari chanya za muktadha zinaweza kufikiwa kwa namna tatu. Kwanza, taarifa mpya iliyozalishwa inaweza kuungana na mabunio au taarifa ya awali aliyonayo mshiriki wa mazungumzo kuzalisha athari za kimuktadha. Pili, taarifa mpya inaweza kuimarisha mabunio ambayo tayari mshiriki wa mazungumzo anayo. Tatu, taarifa mpya inaweza kuwa kuhusika inapokuwa na urari na mabunio ambayo mshiriki wa mazungumzo anayo na matokeo yake taarifa moja inabidi idondoshwe ili kuipa nafasi nyingine. Kimsingi, semi hufasiriwa ndani ya muktadha mahususi wa usemi. Muktadha huo umefasiliwa na Speber na Wilson (1995:15) kama seti ndogo ya mabunio ya mshiriki wa mazungumzo kuhusu ulimwengu pamoja na vipande vyote vya taarifa mpya ambavyo mshiriki wa mazungumzo amewekeza katika mchakato wa ufasiri. Kwa mujibu wa nadharia hii vigeugeu vinavyoathiri muktadha ni vya kijamii, kiutamaduni, kihistoria, ukabila, kiuchumi au hadhi ya mshiriki. Hivi vyote huumba mabunio ya ulimwengu ya mshiriki wa mazungumzo

yanayotumika kupata maana ya usemi inaotakiwa. Mtu anaweza kujiuliza mshiriki wa mazungumzo anachaguaje muktadha wa usemi? Kwa mujibu wa Nadharia ya Uhusiano, vidokezi fulani vya kiisimu katika usemi humwongoza mshiriki wa mazungumzo kuweka mabunio yatakayomsaidia katika mchakato wa ufasiri wa maana. Amfo (2014) anaeleza vidokezo hivyo vya kiisimu katika Nadharia ya Uhusiano vinaitwa visimbusi vya maana ya kiutaratibu. Visimbusi hivyo vinaweza visichangie masharti ukweli au maana ya kidhana bali huashiria njia ya ufasiri wa usemi kwa kudhibiti mchakato wa kung'amua maana (mchakato wa udedushi) iliyokusudiwa ambayo haikuelezwa bayana. Maumbo ya kiisimu katika nadharia hii yameainishwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni la maumbo yenye dhana ya kisemantiki (maana ya kidhana) na kundi la pili ni la semi zinazoangukia kwenye utaratibu wa kisemantiki (maana ya kiutaratibu). Kundi la kwanza linahusisha maumbo yanayowasilisha dhana kama vitenzi, nomino na vivumishi. Maneno hayo ni masharti ukweli kwamba yanaweza kufafanua au kuonyesha tabia ya hali fulani. Kundi la maumbo ya utaratibu wa kisemantiki yanahusisha maumbo yasiyowasilisha dhana bali yanadhibiti namna ukokotozi na kiwakilisho cha akili cha msikilizaji kinavyotakiwa kufanyika katika mchakato wa kuelewa tamko. Maumbo haya humwonyesha msikilizaji aina ya mchakato wa udedushi anaotarajiwa kuupitia katika kufasiri maana. Maumbo haya ya utaratibu wa kisemantiki ndiyo yanayoitwa visimbusi katika Nadharia ya Uhusika.

Baadhi ya watafiti kama Blass (1990), Wilson na Sperber (1993), Andersen na Fretheim (2000), Amfo (2011; 2014) na Otoo (2016) wamechunguza visimbusi mbalimbali vya kiisimu na namna vinavyomwongoza mshiriki wa mazungumzo kufikia fasiri ya maana iliyokusudiwa kwa kudhibiti mchakato wa ufahamu katika kiwango cha maana dhahiri na maana isiyo dhahiri. Katika makala haya Nadharia ya Uhusiano imetumika kubaini visimbusi vya kiisimu vya ufasiri wa mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani na namna visimbusi hivyo vinavyomwongoza mshiriki wa mazungumzo au msomaji wa kilongo kufikia fasiri ya uwakati iliyokusudiwa.

**Mbinu**

Data za makala haya ni sehemu ya data zilizokusanywa na mtafiti katika utafiti wake wa uzamivu. Data hizo zilipatikana katika Maktaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopo mkoani Dodoma, Maktaba Kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili pamoja na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Matini zilizotumika kupata data hizo ni 12 ambazo ni ripoti 2 za serikali, hotuba 2 za viongozi wa serikali, riwaya mbili na magazeti rasmi 6 kutoka kampuni 2. Kati ya matini hizo 12, matini 4 zimetumika kupata data za makala haya. Matini hizo ni hotuba moja (1) ya kiongozi wa serikali, riwaya mbili (2) na gazeti rasmi moja (1). Baada ya kuteua idadi ya sampuli inayohitajika, mbinu ya usampulishaji nasibu sahili imetumika kuteua sampuli wakilishi. Hivyo, majina ya matini zote kumi na mbili (12) yalipewa namba. Kila namba iliandikwa kwenye karatasi yake kisha karatasi hizo zilikunjwa na kuwekwa mezani. Ili kuepuka upendeleo wa aina yoyote kutoka kwa mwandishi wa makala haya, mtu mwingine alipewa kazi ya kuchagua karatasi 4 kati ya karatasi 12 zilizokunjwa. Namba zilizochaguliwa ni ya Hotuba ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya Ufunguzi wa Bunge ya tarehe 20/11/2016, riwaya ya Babu Alipofufuka ya Said A. Mohamed (2007), riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale ya Mohamed Said Abdulla (1997) na gazeti la Mtanzania linalochapishwa na New Habari Ltd la tarehe 30 Aprili 2017.

Data za tungo ambatani kutoka katika matini hizo 4 ndizo zilizotumika kupata data za makala haya. Aidha, data hizo tayari zilikuwa zimepangwa kulingana na kategoria ya vipashio vilivyoambatanishwa na aina ya kiunganishi kilichotumika kuunganisha vipashio hivyo. Hivyo, kwa kuwa makala haya inahusu vishazi ambatani, data zilizochukuliwa kutoka katika matini teule ni zile tu zilizohusu vishazi ambatani vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi kiongezi *na* na kiambishi *-ka-*. Shajara na kalamu zilikuwa zana kuu katika unukuzi wa tungo hizo.

Aidha, data zimechambuliwa kwa kufuata mkabala wa kitaamuli ambao data huwasilishwa kwa kutoa maelezo au ufafanuzi kuhusu vipengele muhimu vilivyolengwa katika utafiti. Hivyo, katika makala haya kipengele kilichofafanuliwa ni mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyobebwa na vishazi ambatani. Ufafanuzi huo ulizingatia kubainisha vidokezo vya kiisimu vinavyomsaidia msomaji au mshiriki wa mazungumzo kufasiri mahusiano uwakati yaliyokusudiwa ambayo hayajaoneshwa kwa uwazi.

**Mahusiano ya Uwakati**

Miongoni mwa mahusiano makuu yaliyopo kati ya vishazi vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi *na* na viunganishi vyingine vyenye dhima sawa na kiunganishi hicho katika lugha mbalimbali ulimwenguni ni mahusiano ya uwakati. Mahusiano haya yapo baina ya vishazi ambatani ambapo tukio au tendo lililoelezwa na kitenzi katika kishazi cha pili limetanguliwa na tukio au tendo lililoelezwa na kitenzi cha kishazi cha kwanza. Hali hii inajibainisha katika mfano namba (3) ambapo mtajwa ambaye ni wafanyakazi, wameiba kwanza viwanja kabla ya kuviuza.

(3) Wafanyakazi wengi [[wameiba viwanja] na [kuviuza kwa watu wengine]]. (Mtanzania 30/4/2017:2)

Kwa mujibu wa nadharia ya uhusika mshiriki wa mazungumzo au mpewa taarifa huunganisha usemi huo wa mfano wa (3) na mswada wa kawaida wa masimulizi pamoja na ulimwengu na maarifa ya kiutamaduni ili kufasiri kuwa tukio la kishazi cha kwanza limetangulia kiwakati tukio la kishazi cha pili. Kwa mfano, katika mfano huo wa (3) mabunio ya kiulimwengu anayokuwa nayo mshiriki wa mazungumzo ni kwamba kabla ya kuuza kitu ni lazima uwe nacho kwanza. Hivyo, ikiwa unapata kitu hicho kwa kuiba ni lazima ukiibe kwanza kabla ya kukiuza. Hii ina maana kwamba, tukio la kuiba viwanja limefuatana kiwakati na tukio la kuviuza. Tazama mfano wa (4) kwa ufafanuzi zaidi.

(4) Watanzania walituchagua na kutupa ridhaa ya kuwaongoza. (Magufuli 20/11/2015:5)

Kwa mujibu wa nadharia ya uhusika, msikilizaji au msomaji wa usemi wa (4) huunganisha mabunio yake ya kiulimwengu na muktadha wa usemi huo ili kufasiri kuwa tukio la kuwachagua lilitangulia kiwakati tukio la kuwapa ridhaa. Hii iko wazi kwamba, kwa maarifa ya kawaida ya kiulimwengu watu huchaguliwa kwanza kabla ya kupewa ridhaa. Huwezi kumpa mtu ridhaa kabla hujamchagua.

Aina hii ya mahusiano ya uwakati yaliyopo baina ya vishazi ambatani vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi *na* na viunganishi vingine vyenye semantiki sawa na kiunganishi hicho yamechunguzwa na watafiti mbalimbali katika lugha mbalimbali. Kwa mfano, Levinson (2000), Carston (2002), Amfo (2007, 2011) na Nartey (2018) wamefafanua namna mahusiano hayo na mahusiano mengine yaliyopo baina ya vishazi ambatani hudokezwa na kufasirirwa na watumia lugha. Watafiti hao, wameeleza kuwa mahusiano hayo hudokezwa kwa kiunganishi ambatanishi chenye semantiki sawa na *na* katika lugha walizochunguza. Tofauti na watafiti hao, Isingoma (2017) na Behrens, Mertins, Hemforth na Fabricius-Hansen (2014) wameonesha kuwa lugha zina namna tofauti za kudokeza mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani. Kwa mfano Isingoma (Keshatajwa) alibaini kuwa katika lugha ya Rotooro kiunganishi ambatanishi '*kandi' na* hakielezi mahusiano ya uwakati bali kina dhima nyingine za kisemantiki kama kusimba maelezo au kufafanua na kudhibiti mchakato wa udedushi unaohusisha viwakilisho vya ubongo. Aidha, ailibaini kuwa mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani katika lugha hiyo hudokezwa na kile kinachoitwa njeo inayofanana na ya wakati uliopo (Vitual Present Tense). (Behrens, Mertins, Hemforth na Fabricius-Hansen, 2014) katika utafiti wao walioufanya katika lugha mbalimbali walibaini kuwa lugha zinatofautiana kwa idadi ya maumbo mbadala yanayotumika kueleza maana mahususi. Wakifafanua maelezo hayo, wanaeleza kuwa wazungumzaji wana mbinu mbalimbali za

kiisimu za kueleza hali ambayo kitajwa kimehusika katika matukio mawili ndani ya sentensi moja. Mbinu hizo huweza kutumika bila kuonyesha kwa uwazi mahusiano ya uwakati baina ya matukio hayo. Mbinu hizo hutofautiana baina ya lugha na lugha, hivyo kwa kuzingatia utafiti wa Isingoma (2017) na Behrens, Mertins, Hemforth na Fabricius-Hansen (2014), makala haya yanachunguza visimbusi vya kiisimu vinavyotumika kufasiri mahusiano ya uwakati ambayo hayajaoneshwa kwa uwazi baina ya vishazi ambatani katika lugha ya Kiswahili.

**Mahusiano ya Uwakati Baina ya Vishazi Ambatani vya Kiswahili**.

Makala haya yamebaini kuwa katika lugha ya Kiswahili kama ilivyo kwa lugha ya Rutooro kiunganishi ambatanishi *na* sio kisimbusi cha mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani. Mahusiano ya uwakati husimbwa kwa kiambishi njeo -*ka*- pamoja na kiambishi kisoukomo *ku*-. Tazama mfano wa (5a na 5b)

(5) a. [[Alikwenda jikoni] na [a**ka**washa moto]]. (Abdulla, 1997:10)
b. [[Alikwenda jikoni] na [**ku**washa moto]].

Katika mfano wa (5a-b) kuna mahusiano ya uwakati baina ya vishazi vilivyoko kwenye mabano. Aidha, semo hizo zinaonesha kuwa kuna uambatanishaji unaomuelekeza mpewa taarifa kuchakata mawazo mawili katika kila usemi kama viambatanishwa. Katika semo hizo, mpewa taarifa atafikia upeo wa ung'amuzi wa uhusiano ikiwa atatumia mahusiano ya udedushi baina ya viambatanishwa kama vile mpangilio kiuwakati. Visimbusi vya kiisimu vinavyomsaidia mpokea taarifa kuweza kufasiri mahusiano husika ya uwakati baina ya vishazi vilivyoambatanishwa katika mfano (5a) ni kiambishi -*ka*- na katika (5b) ni kiambishi ukomo *ku*-.

Kishazi au kiambatanishwa cha pili katika mifano (5a-b) hakiwezi kusimama chenyewe bila msaada wa kisintaksia na kipragmatiki wa kishazi cha kwanza. Utegemezi huo katika kishazi cha kwanza unatawaliwa na njeo iliyotumika ndani yake. Kiambishi -*ka*- kwenye kishazi cha pili katika mifano wa (5a) na kiambishi *ku*- kwenye kishazi cha pili katika mfano wa (5b) vinaonesha kuwa kuna tukio limetokea kabla ya lile lililoelezwa na vishazi hivyo. Kiambishi njeo kilichotumika katika kishazi cha kwanza kina mawanda kwa vishazi vyote viwili katika kila mfano. Hali hiyo inathibitisha kuwa matukio yaliyoambatanishwa yanahusiana kiwakati ambapo yanaweza kuwa yametukia sawia au kwa mfuatano kiwakati. Aidha, mahusiano hayo yanaashiriwa kwa kiambishi -*ka*- katika mfano (5a) na kiambishi *ku*- katika (5b). Viashiria hivyo, humuonyesha mpewa taarifa aina ya mchakato wa udedushi anaotarajiwa kuupitia katika kufasiri maana. Hii ina maana viambishi hivyo ndivyo vinavyoashiria njia ya ufasiri wa usemi kwa kudhibiti mchakato wa udedushi. Hivyo, kishazi chenye kiambishi -*ka*- au -*ku* katika tungo ambatani haviwezi kuanza mwanzoni mwa tungo kama mifano (5c-d) inavyoonesha.

c. *[[A*ka*washa moto]] na [[alikwenda jikoni].
d. *[[*Ku*washa moto]] na [[alikwenda jikoni].

Mifano (5c-d) haikubaliki kisarufi kwa sababu mahusiano ya uwakati yanayodokezwa na viambishi -*ka*- na *ku*- hayapo. Viambishi hivyo, hudokeza kuwa kuna tukio lililotokea kabla ya lile lililoelezwa na vishazi vilivyobeba viambishi hivyo jambo ambalo halidhihirishwa na mifano (5c-d).

**Mahusiano ya Uwakati Yanayodokezwa na Kiambishi -*ka*-**

Kiambishi njeo -*ka*- kama ilivyo katika mfano (5a) ndicho kinachounganisha matukio kiuwakati na sio kiunganishi ambatanishi *na* kama inavyodaiwa kwa viunganishi vyenye semantiki sawa *na* katika baadhi ya lugha. (taz. Carston, 2002; Amfo, 2007, 2011; Nartey, 2018). Kiunganishi *na* kinapotumika katika tungo ambatani yenye kiambishi njeo -*ka*- kama ilivyo kwenye mifano 6, 7, na 8 kinashinikiza maana dhahiri ya ngazi ya juu ambayo ni msisitizo au mshangao. Hivyo, kiunganishi *na* kinapotumika kwenye tungo ambatani yenye kiambishi cha -*ka*- huwa hakiambatanishi matukio bali huonyesha msisitizo au mshangao kama mifano 6, 7, na 8 inavyoonesha.

(6) [[Alikwenda jikoni] **na** [a**ka**washa moto]] (Abdulla, 1997:10)

(7) [[Alifungua sanduku] **na** [a**ka**toa kanga mbili za kwenda kumfunikia muwele]] (Abdulla, 1997:11)

(8) [[Mama Kipwerere anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe], **na** [[**ka**agua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja]]. (Abdulla, 1997:13)

Mifano 6, 7, na 8 inaonyesha kuwa mzungumzaji anaeleza msisitizo ambao ni ngazi ya juu ya maana dhahiri. Mzungumzaji katika mfano wa (6) anasisitiza kuwa mtajwa alienda jikoni, tena baada ya kuenda jikoni hakuishia hapo alifanya tukio lingine la kuwasha moto. Labda haikutarajiwa kuwa mtajwa anaweza kwenda jikoni lakini kinyume na matarajio alienda jikoni tena afanya na tukio la kuwasha moto humo jikoni. Vilevile, katika mfano (7) haikutarajiwa kama mtajwa angeweza kufungua sanduku lakini kinyume na matarajio mzungumzaji anasisitiza kuwa alifungua sanduku tena akatoa kanga mbili. Pia, katika mfano wa (8) inadhaniwa kuwa hakuna mtu anaefahamu maneno ya shetani wa kipwerere. Lakini, kinyume na inavyodhaniwa mzungumzaji anasisitiza kuwa mtajwa ambaye ni mama Kipwerere anafahamu maneno ya shetani wa mwanae na anazidi kusisitiza hilo kwa kueleza kile alichoagua. Tazama mazungumzo kati ya mzungumzaji A na B katika mifano 9, 10, na 11 kwa ufafanuzi zaidi kuhusu suala la msisitizo au mshangao unaodokezwa na kiunganishi na katika mifano 6, 7, na 8.

(9) A: Mgeni hawezi kwenda jikoni
B: Alikwenda jikoni **na** a**ka**washa moto

(10) A: Sidhani kama aliweza kufungua sanduku
B: Alifungua sanduku **na** a**ka**toa kanga mbili za kumfunika muwele

(11) A: Hakuna mtu anafahamu maneno ya shetani wa Kipwerere
B: Mama Kipwerere anafahamu maneno ya shetani wa mwanawe, **na ka**agua kuwa kuna jambo baya mbele yao linakuja.

Katika mfano wa (9) mzungumzaji A anaonekana kukataa au kutoamini ikiwa mgeni anaweza kwenda jikoni. Mzungumzaji B anamueleza kuwa mgeni alikwenda jikoni na kusisitiza kuwa baada ya kwenda jikoni aliwasha moto. Hivyo, kiunganishi *na* katika (9B) kinahitajika kuonesha msisitizo na sio kuambatanisha matukio kwa kuwa kiunganishi ambatanishi ni kiambishi -*ka*-. Pia, katika (10B) na (11B) kiunganishi *na* kinahitajika ingawa uambatanishaji unafanyika kwa kiambishi njeo *-ka-.* Dhima ya kiunganishi *na* ni kumuelekeza mpewa taarifa kwenye hali ya kigambe ya msisitizo. Kwa kuwa *na* na kiambishi -*ka*- vyote ni viunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili haviwezi kutumika kwa pamoja kuambatanisha vipashio viwili. Hali hii imeelezwa na wataalamu mbalimbali kama Dik (1968 34-37), Oirsow (1987:106) kwamba kwa kawaida viunganishi ambatanishi hupishana kimtoano, yaani vipashio viwili haviwezi kuambatanishwa kwa zaidi ya kiunganishi ambatanishi kimoja. Hivyo, ni wazi kuwa kiunganishi *na* na kiambishi njeo -*ka*- vinapoambatana pamoja katika tungo moja haviwezi kufanya kazi ya kuambatanisha kwa pamoja bali kiambishi -*ka*- ndicho huambatanisha ilihali kiunganishi *na* hufanya kazi nyingine kama ya kuonyesha msisitizo. Hivyo, ikiwa mzungumzaji hana lengo la kuonesha msisitizo bali ana lengo la kuonesha kuwa matukio yaliyoambatanishwa yanahusiana kiwakati yaani yametukia kimfuatano, basi kiunganishi *na* huwa hakihitajiki bali hutumika kiambishi -*ka*- peke yake kama mifano (12a-c) inavyonesha.

(12) (a) Najumu kilimjia kicheko, a**ka**cheka. (Abdulla, 1997:15)
(b) Alisimama ghafla, a**ka**tumbua macho mlangoni. (Abdulla, 1997:4)
(c) Shampee ilifunguliwa, i**ka**miminwa kwenye gilasi zake. (Mohamed, 2007:8)

Kiunganishi *na* katika mifano (12a-c) hakikutumika kwa kuwa msemaji hana nia ya kuonyesha msisitizo. Tungo hizo ni tungo ambatani ambazo viambatanishwa vyake vimeambatanishwa kwa kiambisha -*ka*-. Zaidi ya kazi ya kuambatanisha, kiambishi -*ka*- kina dhima nyingine ya kuonesha kuwa matukio yaliyoambatanishwa yanahusiana kiwakati. Kuwapo kwa kiambishi -

*ka*- kunamuelekeza msikilizaji au msomaji aina ya mchakato wa udedushi anaotarajiwa kuupitia katika kufasiri mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa. Kiambishi hicho kinadokeza kuwa matukio yaliyoambatanishwa yanahusiana kiwakati ambapo tukio la pili hufuata tukio la kwanza kiwakati. Hivyo, kuwepo kwa kiambishi hicho kunamwezesha msikilizaji au msomaji kufikia kirahisi fasiri ya uwakati iliyodhamiriwa.

Aidha, Kombe (2019) anaeleza kuwa kiambishi -*ka*- kinapotumika katika dhamira elezi, kishazi cha awali hubeba kiambishi cha njeo iliyopita -*li*- ilhali kinapotumika katika dhamira tegemezi, kishazi cha kwanza huwa na kiambishi cha njeo cha wakati ujao -*ta*-. Hivyo, kiambishi -*ka*- mara nyingi hufuata viambishi njeo -*li*- na -*ta*-. Tazama mfano wa (12) kwa ufafanuzi zaidi.

(13) a. Bwana Msa a**li**sita kwanza, a**ka**koleza mtemba wake, a**ka**wa anavuta. (Abdulla, 1997:65)
b. Ni**ta**enda nyumbani kwa K, ni**ka**mweleze ukweli. (Mohamed, 2007:5)

Katika mfano wa (13a), kishazi cha kwanza kina kiambishi njeo -*li*- kikifuatiwa na mfululizo wa vishazi vyenye kiambishi njeo -*ka*-. Kwa njia hii, mtumiaji wa lugha anaweza kuunda tungo ndefu isiyo na kikomo. Mfano wa (13b) unawakilisha dhamira tegemezi ambapo kishazi cha kwanza kina kiambishi njeo -*ta*- na kishazi cha pili baada ya kupachikwa kiambishi -*ka*-, kiambishi cha dhamira mwishoni kimekuwa -*e*- kumuonesha msomaji au msikilizaji kuwa tukio linalozungumzwa bado halijafanyika bali linatarajiwa kufanyika. Hivyo, kiambishi -*ka*- ni kisimbusi cha kiisimu kinachomsaidia mshiriki wa mazungumzo kung'amua kwamba matukio yaliyobebwa na vishazi vinavyoambatanishwa yapo katika mfuatano kiwakati. Yaani tukio la kishazi cha kwanza hutangulia kiwakati tukio la kishazi cha pili.

**Mahusiano ya Uwakati Yanayoashiriwa na Kiambishi Kisoukomo *ku*-**

Tofauti na kiambika -*ka*- ambacho hufanya kazi kama kiunganishi ambatanishi na kama kisimbusi cha mahusiano ya kiwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa, kiambishi *ku*- hakifanyi kazi kama kiunganishi ambatanishi bali kina dhima moja tu ya kudokeza kuwa matukio yaliyoambatanishwa yanahusiana kiwakati. Suala la dhima ya kiambishi *ku*- kuashiria mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa limewahi kugusiwa na baadhi ya wataalamu kama (Ashton, 1947; Njui, 2015; Riedel na Mark de Vos 2017; Kombe, 2018, 2019). Makala haya yamebaini kuwa kiambishi kisoukomo *ku*- humsaidia msomaji au msikilizaji kusimba mahusiano ya uwakati ya aina mbili. Mahusiano hayo ni yale ya matukio yaliyotukia sawia na yale matukio yaliyofuatana kiwakati. Mifano (14) na (15) inafafanua mahusiano hayo.

(14) [[Chakula kikawa kinameguliwa] **na** [**ku**angamizwa]]. (Mohamed, 2007:42)
(15) [[Ninaviondosha vyakula hivyo] **na** [**ku**wapa majirani waliolala njaa]]. (Mohamed, 2007:38)

Mifano (14) na (15) inaonyesha kuwa vishazi vilivyoko kwenye mabano vimeambatanishwa kwa kiunganishi ambatanishi *na*. Kiambishi kisoukomo *ku*- katika kishazi cha pili kwenye mifano hiyo kinaashiria kuwa, matukio yaliyobebwa na kishazi hicho yanahusiana kiwakati na yale yaliyobebwa na kishazi cha kwanza. Kiambishi kosoukomo *ku*- katika mfano wa (14) kinamsaidia mshiriki wa mazungumzo au msomaji kuweza kufikia fasiri ya mahusiano ya uwakati yaliyokusudiwa baina ya viambatanishwa. Baada ya kutambua kuwa matukio yaliyobebwa na viambatanishwa hivyo yanahusiana kiwakati, muktadha wa kipragmatiki unamsaidia mshiriki wa mazungumzo kuweza kubaini aina ya mahusiano hayo kiwakati. Hivyo, kwa kutumia muktadha wa mawasiliano wa usemi husika, mtu yeyote anaweza kueleza kwamba tukio la kumegua chakula katika mfano wa (14) linatukia sawia na tukio la kukiangamiza. Yaani tukio la kumegua chakula na tukio la kuangamia kwa chakula yanatukioa wakati mmoja. Kwa kawaida mshiriki wa mazungumzo anakuwa na mabunio ya kiulimwengu kuwa kadri chakula kinavyozidi kumeguliwa ndivyo kinavyozidi kuisha yaani kuangamizwa. Hivyo, mabunio hayo pamoja na kisimbusi *ku*- vinamsaidia mshiriki wa mazungumzo au

msomaji kubaini mahusiano ya uwakati yaliyokusudiwa baina ya vishazi vilivyoambatanishwa. Hivyo, mahusiano ya uwakati yaliyopo baina ya tukio la kiambatanishwa cha kwanza na tukio la kiambatanishwa cha pili ni uhusiano wa kutukia sawia.

Vilevile, kwa kutumia muktadha wa mawasiliano wa tamko, mshiriki wa mazungumzo au msomaji atabaini kuwa tukio la kuwapa chakula majirani katika mfano wa (15) linafuata kiwakati baada ya kukiondosha. Hivyo, mahusiano ya uwakati baina ya tukio la kishazi cha kwanza na cha pili katika mfano wa (15) ni uhusiano wa kutukia kimfuatano ambapo tukio la kishazi cha pili linafuata kiwakati baada ya tukio la kishazi cha kwanza. Kiunganishi *na* katika mifano (14) na (15) kinahitajika kuunganisha viambatishwa lakini mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa yanadokezwa kwa kiambishi *ku*-. Kiunganishi *na* hakiwezi kuonesha mahusiano ya uwakati kutokana na semantiki yake. Katika Semantiki Rasmi Behrens, Mertins, Hemforth na Fabricius-Hansen (2014) wanaeleza kuwa, kiunganishi hicho ni kiunganishi mantiki au shirikishi cha matendo (ungano, jumla) kulingana na aina ya semantiki ya hoja yake. Kutokana na ufafanuzi huo wanaendelea kueleza kwamba, kiunganishi '*and*' *na* hakiwezi kudhibiti mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoelezwa katika viambatanishwa viwili.

Aidha, Ashton (1947) anadai kwamba kiambishi kisoukomo *ku*- hutumika katika tungo ambatani ikiwa tukio la kishazi cha pili si matokeo ya tukio la kishazi cha kwanza, au si matukio yanayofuatana kiwakati. Madai hayo Ashton yamepigwa na (Kombe 2018, 2019), anayeleza kuwa hakuna mipaka hiyo kwani kishazi cha pili huwa kishazi kisoukomo hata kama tukio la kishazi cha pili ni matokeo ya tukio la kishazi cha kwanza au ni matukio yanayofuatana kiwakati. Maelezo ya Kombe (keshatajwa) yanathibitishwa na data za makala haya zinazoonesha kuwa kiambishi kisoukomo huonyesha mahusiano ya kufuatana kiwakati baina ya matukio ambatani. Hivyo, katika makala haya imebainika kuwa kiambishi kisoukomo *ku*- humsaidia mshiriki wa mazungumzo kubaini mahusiano ya uwakati bila mipaka iliyoelezwa na Ashton (Keshatajwa). Tukirejea mfano wa (15), kishazi cha pili ni kishazi kisoukomo yaani kina kiambishi kisoukomo *ku*- na matukio yaliyobebwa na vishazi hivyo yanauhusiano wa mfuatano kiwakati. Aidha, kama mfano wa (16) unavyoonesha matukio yaliyobebwa na viambatanishwa vilivyoko kwenye mabano yana mahusiano ya usababishi ambapo tukio la kishazi cha pili ni matokeo ya tukio la kishazi cha kwanza. Pamoja na mahusiano hayo ya usababishi baina ya matukio hayo, bado kiambishi kisoukomo *ku*- katika kishazi cha pili kinadokeza mahusiano uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa.

(16) [[Bomba limepasuka] **na** [**ku**bwabwaja maji]] (Mohamed, 2007:41)

Kishazi cha kwanza katika mfano wa (16) ni kishazi ukomo na kishazi cha pili ni kishazi kisoukomo. Kwa kutumia mabunio ya kiulimwengu ni wazi kuwa tukio la kubwabwaja maji ni matokeo ya kupasuka kwa bomba. Hii ina maana tukio la bomba kubwabwaja maji limesababishwa na tukio kupasuka kwa bomba. Hivyo, tukio la kubwabwaja maji limefuata baada ya tukio la bomba kupasuka. Hii ina maana tukio la bomba kupasuka na tukio la bomba kubwabwaja maji yana mahusiano ya kiwakati. Mhusiano hayo ya uwakati yamedokezwa na kiambishi kisoukomo *ku*- kilichopo katika kishazi cha pili. Hali hiyo inathibitisha kuwa kiambishi kisoukomo *ku*- hudokeza mahusiano ya uwakati hata kwa matukio yenye uhusiano wa kiusababishi.

**Vishazi Ambatani Visivyo na Visimbusi vya Uwakati**.

Tumeona kwamba kishazi kinachobeba visimbusi vya kiisimu vinavyodokeza mahusiano ya uwakati yaani kiambishi -*ka*- na *ku*- huwa hakina kiambishi njeo bali hutegemea njeo ya kishazi cha kwanza. Utegemezi huo kudhihirisha kuwa tukio la kishazi cha pili hutegemea kiwakati tukio la kishazi cha kwanza. Hii ina maana uwepo wa kiambishi -*ka*- au kiambishi *ku*- kuashiria mahusiano baina ya viambatanishwa viwili ni wazi kuwa vikikosekana matukio yaliyobebwa na viambatanishwa hivyo yataeleweka tu kama matukio tengani ambayo kila

moja limetukia au litatukia kwa wakati wake na katika muktadha tofauti. Kwa ufafanuzi zaidi tazama mifano (17a-b)

(17) a. [[Mna wa**na**otaka usawa] na [wa**na**opinga usawa]]. (Mohamed, 2007:46)
b. [[A**li**endelea kudai kuwa ni mwenyekiti halali], na [a**li**zidisha msimamo wake]]. (Mtanzania 30/5/2017:4)
c. [[[Tu**me**ingia kwenye uchaguzi wamoja], [tu**me**shindana katika kampeni tukiwa wamoja], na tu**me**maliza uchaguzi wetu tukiwa wamoja]]] (Magufuli 20/11/2015:8)

Kila kishazi katika mifano (17a-c) kina kiambishi njeo kilichokolezwa wino. Aidha, kiambishi Viambishi hivyo vilivyoko katika kishazi cha kwanza na cha pili katika kila vinathibitisha kuwa matukio yaliyoambatanishwa hayana uhusiano wowote kiwakati kwani kila tukio limetukia kwa wakati wake na huenda yalitukia katika miktadha tofauti. Suala hilo limeelezwa pia na Kombe (2018) akimrejelea Njui (2015) kwamba ikiwa kila kishazi katika tungo ambatani kitakuwa na kiambishi njeo katika muundo wa nje, matukio yaliyobebwa na vishazi hivyo yatakuwa hayahusiani kipragmatiki. Njui anaeleza kuwa matukio hayo hayahusiani kipragmatiki kwa sababu hakuna alama yoyote inayoashiria uhusiano wa kiwakati au wa aina nyingine yoyote kati ya matukio hayo. Hivyo, kutokuwepo kwa kidokezo chochote cha uhusiano wa uwakati katika mifano (17a-c) inamuwia vigumu mshiriki wa mazungumzo au msomaji kufikia fasiri ya mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa. Hata hivyo, uwepo wa kiambishi njeo katika kila kishazi katika mifano (17a-c) ni ishara kwa mshiriki wa mazungumzo kuwa matukio yaliyoambatanishwa hayahusiani kiwakati kwani kila tukio lilitukia kwa wakati wake.

**Mpangilio wa Viambatanishwa Vyenye Matukio Yanayohusiana Kiwakati**
Visimbusi vya uwakati tulivyojadili katika makala haya ambavyo ni kiambishi *-ka-* na *ku-* hupachikwa katika kiambatanishwa cha pili kwa tungo ambatani zenye viambatanishwa viwili. Aidha, Kombe (2019) anaeleza kuwa, tungo ambatani zenye viambatanishwa zaidi ya viwili hupachikwa kwenye viambatanishwa vyote isipokuwa kiambatanishwa cha kwanza. Visimbusi vya uwakati *-ka-* na *ku-* hufanya tungo ambatani kuwa na mpangilio wa viambatanishwa usiobadilika. Jaribio lolote la kujaribu kubadili nafasi za viambatanishwa katika tungo ambatani husababisha tungo isiyokubalika kisarufi kwa sababu mahusiano ya uwakati yanayodokezwa na viambishi hivyo. Mifano (18) na (19) inafafanua zaidi suala la mpangilio wa vishazi au viambatanishwa vyenye viambishi *-ka-* na *ku-* ambavyo vinaashiria mahusiano ya uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa.

(18) *Kubabwaja maji na bomba limepasuka
(19) *Akawasha moto na alikwenda jikoni

Kwa kutumia muktadha wa mawasiliano msomaji anaweza kueleza kuwa mifano (18) na (19) haikubaliki kisarufi. Tungo hizo zimepoteza usahihi wake kisarufi kwa sababu matukio yaliyobebwa na viambatanishwa yalikuwa yanafuatana kiwakati. Hivyo, tukio la pili haliwezi kuanza kabla ya tukio la kwanza. Aidha, vishazi vyenye matukio yaliyo katika mfuatano maalumu kiwakati au yenye mahusiano ya kiusababishi huwa na mpangilio usiobadilika. Kwa mfano, kishazi chenye tukio linalosababisha tukio lingine ni lazima kiwe cha kwanza katika tungo ambatani kikifuatiwa na kishazi chenye tukio lililosababishwa. Vilevile, visimbusi vya ufasiri wa mahusiano ya uwakati hupachikwa kwenye kitenzi cha kishazi cha pili ili kuonesha kuwa tukio la kishazi hicho linategemea tukio la kishazi cha kwanza kiwakati. Kutokana na utegemezi huo, mpangilio wa vishazi ambatani ukibadilishwa kama ilivyo katika mfano (18) na (19) huzalisha tungo zisizokubalika kisarufi. Aidha, ikiwa matukio yaliyobebwa na vishazi ambatani hayana mahusiano yoyote kiwakati, mpangilio wa viambatanishwa huweza kubadilika bila kuathiri maana au usarufi wa tungo husika. Mifano 20 na 21 inathibitisha suala hilo.

(20) a [[Najumu a**me**jinyoosha] na [a**me**fumba macho]]. (Abdulla, 1997:9)

b. [[Najumu a**me**fumba macho] na [a**me**jinyoosha]].

(21) a. [[Tu**me**ingia kwenye uchaguzi wamoja], [tu**me**shindana katika kampeni tukiwa wamoja], na tu**me**maliza uchaguzi wetu tukiwa wamoja]]] Magufuli 20/11/2015:8)

b. [[[Tu**me**maliza uchaguzi wetu tukiwa wamoja], [tu**me**shindana katika kampeni tukiwa wamoja] na [Tu**me**ingia kwenye uchaguzi wamoja]]

Mifano (20b) na (21b) inaonyesha kuwa mpangilio wa viambatanishwa au vishazi vilivyoambatanishwa umebadilishwa tofauti na mpangilio ulivyokuwa katika mifano (20a) na (21a). Hata hivyo, pamoja na mpangilio huo kubadilishwa tungo zilizozalishwa bado inakubalika kisarufi. Kukubalika kisarufi kwa tungo hizo hata baada ya mpangilio kubadilishwa kunathibitisha kuwa matukio yaliyoambatanishwa katika tungo hizo hayana uhusiano wowote kiwakati. Hali hii ni tofauti kwa tungo zenye matukio yanayohusiana kiwakati kama tulivyoona katika mifano (18) na (19.)

## Hitimisho

Makala haya yamechunguza visimbusi vya kiisimu vinavyomsaidia mshiriki wa mazungumzo au msomaji kufikia ufasiri wa mahusiano ya uwakati yaliyokusudiwa baina ya vishazi ambatani vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi *na* katika lugha ya Kiswahili. Katika makala haya ufafanusi wa kina umetolewa kuhusu visimbusi vya ufasiri wa mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani vilivyoambatanishwa kwa kiunganishi *na*. Makala imeonyesha kuwa, kiunganishi ambatanishi *na* hakina dhima ya kipragmatiki ya kudokeza mahusiano ya uwakati baina ya vishazi ambatani katika lugha ya Kiswahili kama ilivyo kwa viunganishi vyenye semantiki sawa na *na* katika baadhi ya lugha (taz. Levinson, 2000; Carston, 2005; Amfo, 2007, 2011; Nartey, 2018). Makala haya yameonesha kuwa, kiunganishi hicho kinapofuatana na kiambishi njeo -*ka*- huwa na dhima ya kipragmatiki ya kuonesha msisitizo ilihali kiambishi -*ka*- ndicho huambatanisha matukio na kudokeza mahusiano ya uwakati. Mahusiano hayo ni ya mfuatano maalum kiwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa. Tofauti na kiambishi -*ka*- imeelezwa kuwa kiambishi kisoukomo *ku*- chenyewe hakiambatanishi matukio bali kina dhima moja tu ya kipragmatiki ya kudokeza mahusiano wa uwakati baina ya matukio yaliyoambatanishwa. Hivyo, kiambishi *ku*- hakiwezi kuonyesha mahusiano hayo ya uwakati pasipo kiunganishi ambatanishi *na* ambacho huambatanisha viambatanishwa ilhali kiambishi -*ka*- kinaweza kuonyesha mahusiano hayo bila kiunganishi ambatanishi *na* kwa kuwa chenyewe ni kiunganishi ambatanishi. Mahusiano ya uwakati yanayodokezwa na kiambishi *ku*- ni mahusiano ya matukio kufuatana kiwakati na mahusiano ya matukio kutukia kwa wakati mmoja kiwakati.

## Marejeleo


Abdulla, M. S. (1997). Mzimu wa Watu wa Kale. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Amfo, N. A. A. (2007). Clausal Coordination in Akan. *Lingua* 117, 666-684

Amfo, N. A. A. (2011). The Dangme clausal connective nɛ. *Journal of West African Languages XXXVIII*(1), 53-68

Andersen, G. na Thorstein F. (2000). *Pragmatic markers and propositional attitude.* Pragmatics and Beyond, New Series. Amsterdam: John Benjamins.

Ashton, E. O. (1947). *Swahili grammar*. London: Longmans Group Limited.

Assimakopoulos, S. (2015). Motivating the procedural analysis of logical connectives. *Nouveaux Cahiers de Linguistique Française* 32, 59-70.

Blakemore, D. (1987). *Semantic Constraints on Relevance*. Oxford: Blackwell.

Blakemore, D. na Carston, R. (2005). The pragmatics of sentential coordination with ‘and’. *Lingua* 115, 137-146.

Blass, R. (1990). *Relevance relations in discourse: A study with special reference to Sissala*. Cambridge: Cambridge University Press

Behrens, B., Schmiedtová, B., Hemforth, B., na Fabricius-Hansen, C. (2014). Understanding coordinate clauses: A cross-linguistic experimental approach. Katika B. Hemforth, B. Schmiedtová, & C. Fabricius-Hansen (Eds.). *Psycholinguistic approaches to meaning*

*and understanding across languages* (Studies in theoretical psycholinguistics, kur. 23– 51). Cham: Springer.
Carston, R. (1993). Conjunction, explanation, and relevance. *Lingua* 90: 27–48.
Carston, R. (2002). *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Oxford: Blackwell.
Dik, S. C. (1968). *Coordination: Its Implications for the Theory of General Linguistics*. Amsterdam: North-Holland Publishing Company.
Forceville, C. (2005). Addressing an audience: Time, place, and genre in Peter Van Straaten's calendar cartoons. *Humor* 18: 247–78.
Forceville, C. (2014). Relevance theory as a model for analyzing visual and multimodal communication. In *Visual Communication*. Handbooks of Communication Science. No. 4. Edited by Machin, David. Berlin: De Gruyter Mouton, pp. 51–70.
Grice, Paul. (1967). *Logic and conversation.* William James Lectures; Cambridge: Harvard University.
Haspelmath, M. (2000). Coordination. Katika Timoth, S. (mh), *Language typology and linguistic description* (Toleo la 2) Cambridge: Cambridge University Press.
Haspelmath, M. (2004). *Coordinating Constructions*. Amsterdam: John Benjamins.
Isingoma, B. (2017). The pragmatics of Kandi: A relevance-theoretic account. *Argumentum, 13*, 174-184
Kombe, L. E. (2019). *Uchambuzi wa Sintaksia ya Uambatanishaji katika Lugha ya Kiswahili*, University of Dar es Salaam. Unpublished Ph.D. Dissertation.
Kombe, L. E. (2018). Uambatishaji wa Vishazi katika Lugha ya Kiswahili: Uchunguzi wa Madai ya De Vos na Riedel (2017)' *Kioo cha lugha 16*(1), 153-164
Levinson, S. (2000). *Presumptive meanings: The theory of generalized conversational implicature*. Cambridge: MIT Press.
Magufuli, J. P. J. (2015). Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dodoma: Ikulu.
Mithun, M. (1988). "The grammaticalization of coordination. Katika *Typological Studies in Language* (Toleo la 18) John Benjamins.
Mohamed, S. A. (2007). Babu Alipofufuka. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.
Mtanzania (2017). Toleo Na. 8531. Dar es Salaam. New Habari Ltd.
Nartey, M. (2018). Clausal Coordination in Gã: The Case of nì. *Languages* 3 (3), 1-13
Njui, M. M. (2015). Coordination and subordination in the Kenyang Language. *Journal of Foreign Languages, Cultures, and Civilizations* (Juz. 3) kur. 8-14 https://www.researchgate.net/publication/281669738.
Oirsouw, R. (1987). *The Syntax of coordination*. London: Croom Helm.
Otoo, R. (2016). The pragmatics of the marker 'kulɛ' in utterance interpretation: The case of Gã. *Research on Humanities and Social Sciences* 6: 77–86.
Riedel, K. na Mark de Vos, A. (2017). "Swahili coordinated infinitives and noncanonical case-marking", Katika *African Languages and Linguistics*, 38 (2): kur. 265-288.
Sperber, D. na Deirdre W. (1995). *Relevance: communication and cognition* (2nd ed.). Blackwell publishing. 2nd edition.
Wilson, D. na Sperber, D. (1993). Linguistic form and relevance. *Lingua* 90, 1-25.
Wilson, D. na Sperber, D. (2004). Relevance theory. In Horn, L.R. & Ward, G. (eds.). *Handbook of Pragmatics*. Oxford: Blackwell, 607-632.